JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KAHAWA TANZANIA

(Imeanzishwa kwa Sheria ya Kahawa Namba 23 ya Mwaka 2001 na Marekebisho ya Sheria za Mazao Na. 20 ya mwaka 2009)

MWONGOZO WA KWANZA WA UPATIKANAJI WA MBOLEA KWA WAKULIMA WA KAHAWA

Mwongozo huu umetolewa chini ya sheria ya tasnia ya Kahawa Na. 23 ya mwaka 2001 na marekebisho yake Ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2013

Umetolewa na:
Bodi ya Kahawa Tanzania,
S. L. P. 732,
MOSHI.

Agosti, 2021.

YALIYOMO ……..……..i

TAFSIRI NA MAANA YA VIFUPISHO VYA MANENO……ii

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI ……..…….1

SEHEMU YA PILI

2.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO.....2

SEHEMU YA TATU

3.0 MAJUKUMU YA WADAU WA MPANGO ……..….5

SEHEMU YA NNE

4.0 MAMBO YA JUMLA..... 9

TAFSIRI YA VIFUPISHO NA MAANA ZA MANENO YALIYOTUMIKA

AMCOS	Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko
CHAMA	Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko
TCB	Tanzania Coffee Board
TFRA	Tanzania Fertilizer Regulatory Authority
TaCRI	Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania
VEO	Afisa Mtendaji wa Kijiji
VAEO	Afisa kilimo wa kijiji (Bwana shamba wa kijiji)
WEO	Afisa Mtendaji wa Kata
WAEO	Afisa kilimo wa Kata (Bwana shamba wa kata)
RAA	Mshauri wa Kilimo wa Mkoa
UNION	Chama Kikuu cha Ushirika
RCS	Chama cha Ushirika cha Msingi
TCDC	Tume ya Maendeleo ya Ushirika

1.0 UTANGULIZI

Bodi ya Kahawa Tanzania, kwa mujibu wa Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kahawa ya mwaka 2013 inatoa mwongozo huu kwa wadau wa kahawa ili kutekeleza mpango wa upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wa kahawa. Mpango huu una lengo la kuongeza upatikanaji na matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji.

Matumizi madogo na yasiyo sahihi ya mbolea za viwandani ni moja ya vikwazo vilivyotajwa katika kuongeza tija na uzalishaji wa kahawa kwa wakulima wadogo. Sababu kubwa ya matumizi madogo ya mbolea ni kukosekana kwa mfumo ulio rasmi unaowahakikishia wakulima wa kahawa kupata mikopo nafuu kwa ajili ya upatikanaji wa mbolea. Wakulima wanalazimika kutegemea mikopo inayotolewa na wafanyabiashara katika maeneo yao, makampuni binafsi na taasisi nyingine zisizo za kifedha ambazo wanapaswa kulipa kwa riba kubwa au kwa kulipia kahawa (cherry). Hivi sasa tija katika uzalishaji wa kahawa ni ndogo na inakadiriwa kuwa Kilogramu 150-200 kwa hekta kwa kahawa aina ya Arabika au takribani Gramu 150 kwa mti ikilinganishwa na Kilogramu 800-1500 kwa hekta na gramu 800 - 1000 kwa mti mmoja wa kahawa inayopatikana kwenye mashamba makubwa ambayo yana matumizi yanayoridhisha ya pembejeo za kilimo pamoja na kanuni bora za zao la kahawa

1.2 Lengo la Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kutoa utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa upatikanaji na usambazaji wa mbolea kwa wakulima wadogo wa kahawa kwa kila mwaka. Maelekezo yametolewa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mpango huu kama vile mbolea zitakazohusika kwenye mpango, utaratibu wa ukusanyaji wa takwimu za mahitaji ya mbolea, utaratibu wa upatikanaji wa mikopo, ununuzi na usambazaji wa mbolea, urejeshaji wa mikopo, usimamizi ufuatiliaji na tathimini ya mpango. Aidha, majukumu mbalimbali ya kila mdau yameelezwa ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuongeza kasi ya uzalishaji kahawa nchini. Hivyo ni jukumu la kila mdau kuhakikisha anatimiza wajibu wake katika kuendeleza Tasnia ya Kahawa nchini kwa kuzingatia mwongozo huu.

Kwa mujibu wa mwongozo huu neno “Mkulima” linajumuisha mkulima binafsi, Chama Kikuu cha Ushirika (Union) na Vyama vya Msingi (Agricultural Marketing and Cooperative Socities – AMCOS). Aidha, na neno “Chama” litamaanisha “Chama Kikuu cha Ushirika na Vyama vya ushirika vya Msingi (AMCOS)kama inavyotafsiriwa kwa mujibu wa sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

SEHEMU YA PILI

2.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO

2.1 Utekelezaji wa mpango

Utekelezaji wa mpango huu wa upatikanaji wa mbolea utakuwa kama ifatavyo:

(i) **Utambuzi wa wakulima:** Kila chama cha ushirika cha msingi kitatayarisha ya wakulima ambayo itakuwa na taarifa muhimu za wakulima ikiwa ni pamoja na majina yao, sehemu, ukubwa wa mashamba yao na idadi ya miti ya kahawa waliyo nayo.

(ii) **Wakulima:** Kila mkulima atawasilisha kwenye chama chake cha Msingi (AMCOS) kiasi cha mbolea kinachohitajika kwa mahitaji ya shamba lake kulingana ukubwa wa shamba lake la kahawa na idadi ya miti ya kahawa.

(iii) **Chama cha Msing (AMCOS)** kitakusanya mahitaji yote na kuwasilisha kwenye Chama Kikuu cha Ushirika kama kinafanya shunguli zake kupitia chama kikuu na kama kinajitegemea kitapeleka mahitaji yake moja kwa moja kwa Mwezeshaji waliomchagua katika eneo lao.

(iv) **Vyama Vikuu vya Ushirika**: Vitakusanya na kuthibitisha mahitaji ya mbolea ya wanachama wake na kuanza taratibu za kuomba mkopo.

(v) **Muwezeshaji/Mtoa huduma (Financier):** Atatayarisha mkopo (credit facility) au dhamana ya mkopo (credit guarantee) kwa chama husika na kuiwasilisha kwa msambazaji husika wa pembejeo kulingana na masharti na taratibu zilizokubaliwa.

(vi) Mkopaji/Chama Kikuu cha Ushirika au (AMCOS) kitasaini makubaliano ya pande tatu/nne kati ya Bodi ya (TCB), mtoa huduma (Wakala wa Pembejeo), mwezeshaji (Financier) pamoja na msambazaji mbolea. Makubaliano hayo yenye taarifa za akaunti ya malipo itakayotumika kurejesha mkopo pia yatatoa idhini (consent) kwa Bodi ya Kahawa kukata kiasi cha malipo ya kahawa kwa wauzaji wa kahawa kwenye minada ya kahawa na kumlipa mtoa huduma.

(vii) **Msambazaji wa Mbolea:** Atahakikisha kiasi cha mbolea kilichokubaliwa kinafika kwenye chama husika kulingana na mahitaji.

(viii) **Halmashauri za Wilaya:** Kuhakiki endapo maombi ya kila Chama kama yanaendana na uwezo wa uzalishaji na pia kutoa huduma za ugani kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya mbolea.

2.2 Aina za mbolea zitakazotumika na kusambazwa

Katika kutekeleza mpango huu aina za mbolea zitakazotumika ni zile zilizopendekezwa kutumika katika eneo husika na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI). Pia taasisi ya utafiti wa kahawa imependekeza viwango vya matumizi (application rate/acre/tree) kwa kila eneo/kanda linazozalisha kahawa kulingana na aina ya udongo wa eneo husika.

Mbolea hizi ni kama ifuatavyo;

Kanda	Aina ya Mbolea	Kiwango cha matumizi
Songwe/Mbeya	NPK 22:6:12+3S	60 g/mti mara 3 kwa mwaka
Kaskazini	NPK 22:6:12+3S	90g/mti, mara 2 kwa mwaka
Ruvuma	NPK 15:9:19+3S	80 g/mti mara 3 kwa mwaka
Kigoma	NPK 15:9:19+3S	120g/mti, mara 2 kwa mwaka.
Kagera	NPK 22:6:12+3S,	80 g/mti mara 3 kwa mwaka

Wakulima wameshauriwa kutumia mbolea hizi pamoja na mbolea za Minjingu Asilia 50g/mti/mwaka na mbolea za kunyuzia kwenye majani (Foliar fertilizer) 20:20:20 +micronutrients, mara 2 kwa mwaka. Aidha wakulima watakuwa huru kuchagua msambazaji au mtoa huduma yeyote atakayewapa huduma nzuri kwa bei nafuu katika eneo lao lakini mbolea yenye ubora. Aidha, vyama vya ushirika vinashauriwa kuratibu na kuweka mipango ya kuwawezesha wakulima kupima afya ya udongo kwenye mashamba ya kahawa hususaniviwango vya tindikali (pH) na kufanya matibabu stahiki ili mbolea zitakazowekwa katika miti ya kahawa zifanye kazi kwa ufanisi. Kwa udongo wenye pH ndogo chini ya 7 wakulima wanashauriwa kuweka chokaa (liming) ili mbolea za ziada zitakazowekwa zifanye kazi kwa ufanisi.

2.3 Ukusanyaji wa mahitaji ya mbolea kutoka kwa wakulima

i. Vyama vya ushirika (AMCOS, RCS) vitakusanya takwimu za mahitaji ya mbolea kutoka kwa wanachama wake kwa kushirikiana na maafisa ugani walio katika maeneo yao.

ii. Vyama vitahakiki na kuthibitisha takwimu za mahitaji ya mbolea ya wanachama wake.

iii. Baada ya kupata takwimu za mahitaji ya vyama vya ushirika vitaanza utaratibu wa kuomba mikopo kwa mujibu wa sheria.

iv. Pia chama husika kitaanza utaratibu wa kuomba mkopo kwenye mabenki, taasisi za kifedha au wawezeshaji (Makampuni, wenye Viwanda n.k) kulingana na kiasi cha mbolea kinachohitajika.

v. Halmashauri za Wilaya kupitia maafisa Kilimo/ushirika zitahakiki maombi ya kila chama kama yanaendana na uwezo wa uzalishaji.

Shughuli zote zitafanyika kulingana na Kalenda ya Kilimo kwa zao la kahawa katika eneo husika na hatua ya ukuaji

2.4 Utaratibu wa Mikopo ya upatikanaji wa mbolea

i. Kabla ya msimu wa kilimo cha kahawa kuanza chama husika kitawasiliana na watoa huduma ya mikopo ya mbolea ili kuweza kuchagua mtoa huduma mwenye huduma bora.

ii. Watakaohusika kutoa huduma ya mikopo ya mbolea watakuwa hawa wafuatao;

(a) Taasisi za kifedha mf. Benki, SACCOS,

(b) Wawezeshaji wengine (makampuni binafsi, wenye viwanda n.k) kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba (contract farming) kama ilivyoanishwa katika kanuni ya 59 (1) ya kanuni za kahawa za mwaka 2013.

(c) Wasambazaji wa pembejeo (Agro-dealers).

(d) Wenye mashamba makubwa kupitia *Out growers' schemes.*

iii. Baada ya kukubaliana na mtoa huduma, chama cha ushirika kitajaza mkataba wa makubalino ya kupewa mkopo na taasisi/mtoa huduma husika (**Kiambatisho I)** na kuiwasilisha kwenye ofisi ya Mrajisi wa Ushirika (Mkoa/Wilaya) kwa ajili ya uhakiki na kupitishwa.

iv. Baada ya kupitishwa kwa makubaliano hayo maombi hayo yatawasilishwa Bodi ya Kahawa kwa ajili ya kupitiwa na kusajiliwa kwa mujibu wa kanuni ya 59 (3) na kufuatilia utekelezwaji wake.

2.5 Usambazaji wa mbolea kwa wakulima

i. Baada ya makubaliano kukamilika chama husika kitawasilisha makubaliano hayo kwa msambazaji wa mbolea ili atayarishe kiasi cha mbolea kilichokubaliwa na kukifikisha moja kwa moja kwenye chama husika kulingana na makubaliano ya mkataba na kalenda ya kilimo cha kahawa katika eneo husika.

ii. Chama husika cha Ushirika kitawagawia wanachama wake kiasi cha mbolea kulingana na mahitaji ya kila mwanachama.

iii. Hakuna mkopo wa ununuzi wa mbolea utakaotolewa moja kwa moja kwa mkulima kama fedha taslimu bali kiasi cha mbolea kilichoombwa.

2.6 Urejeshaji wa mikopo ya ununuzi wa mbolea

i. Urejeshwaji wa malipo ya mbolea utafanyika wakati wa mauzo ya kahawa kulingana na kiasi ambacho kila chama kilivyokopa.

ii. Bodi ya Kahawa itaelekeza malipo ya chama husika kwenye akaunti ya mkopaji ambayo ilikubaliwa wakati wa kuingia makubaliano.

iii. Bodi ya Kahawa haitatoza gharama yeyote kwa huduma ya urejeshaji wa mikopo ya mbolea.

2.7 Faida zitakazotokana na utekelezaji wa mfumo huu

i. Kuongezeka kwa tija na uzalishaji wa kahawa.

ii. Ufanisi na kuboresha utoaji huduma.

iii. Kupunguza gharama ya upatikanaji wa Mbolea.

iv. Kuhakikisha upatikanaji wa mbolea inayofaa kwenye zao la kahawa kwa kiwango kinachohitajika na kwa wakati.

v. Kuongeza ubora wa kahawa inayozalishwa na mkulima.

vi. Kujenga mtandao wa ushirikiano wa kitaasisi ili kuwa na sekta endelevu.

vii. Kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi za matumizi ya mbolea.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO

Majukumu ya wadau katika kutekeleza mpango huu yameainishwa kama ifuatavyo:

3.1 Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB)

Majukumu ya Bodi ya Kahawa katika utekelezaji wa mpango ni kama ifuatavyo:-

i. Kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa mbolea kwa wakulima kwa mujibu wa sheria.
ii. Kuratibu utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wa Kahawa.
iii. Kusajili makubaliano na mikataba ya upatikanaji wa mbolea kati ya vyama vya ushirika, watoa huduma na taasisi nyingine. Kupokea na kutunza taarifa zote za mbolea iliyosambazwa kwa wakulima wa Kahawa.
iv. Kuhakikisha mikopo ya mbolea inarejeshwa kwa wakati kupitia mauzo ya kahawa ya vyama husika.
v. Kutatua changamoto zitakazojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu kwa kuzingatia kifungu nambari 76 (1) cha kanuni za Kahawa za mwaka 2013.
vi. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mpango wa mbolea kwa kushirikiana na wadau wengine.

3.2 Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI)

Majukumu ya TaCRI katika utekelezaji wa mpango huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya utafiti na kutoa ushauri wa aina za mbolea zinazohitajika kwa eneo husika;
(ii) Kusaidia kufanya tathimini ya udongo kwenye mashamba ya kahawa kujua upungufu wa virutubisho vinavyohitajika.
(iii) Kutoa elimu na ujengaji wa uwezo kwa Halmashauri za wilaya juu ya umuhimu wa matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa kahawa walio katika maeneo yao.
(iv) Kutoa elimu kwa Maafisa ugani, wakulima, viongozi na wazalishaji umuhimu wa matumizi ya mbolea katika kuongeza tija ya uzalishaji wa kahawa.

3.3 Mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa Mbolea (TFRA)

Majukumu ya taasisi ya usimamizi wa mbolea ni kama yafuatayo:

i. Kutoa elimu ya namna ya ununuzi na uagizaji wa mbolea kwa wadau wa kahawa.

ii. Kutoa elimu na kuhamasisha juu ya mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja (Bulk procurement) ambao wakulima kupitia vyama vyao vya ushirika wanaweza kuutumia kuagiza mbolea na kuipata kwa gharama nafuu na kwa wakati.

iii. Kushirikiana na taasisi ya utafiti wa kahawa (TaCRI) kutoa ushauri wa kitalaamu juu ya aina za mbolea, kupendekeza na kuhamasisha matumizi ya mbolea sahihi kwa kilimo cha kahawa.

3.4 Ofisi za Sekretariet za Mikoa

i. Kushiriki katika kampeni za uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima.

ii. Kuratibu shughuli zote za utekelezaji wa mpango huu katika Mkoa husika.

3.5 Halmashauri za Wilaya

Majukumu ya Halmashauri za Wilaya ni kama yafuatavyo:

(i) Kufanya tathimini ya kiasi cha mahitaji ya mbolea kwa wakulima yaliyowasilishwa na vyama vyao vya ushirika.

(ii) Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa matumizi ya mbolea kwa wakulima na kuhakikisha mbolea inatumika kama inavyotakiwa kwenye zao la kahawa na si vinginevyo.

(iii) Kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi bora ya mbolea.

(iv) Kuwasilisha Bodi ya Kahawa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wa kahawa.

(v) Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu

3.6 Wawezeshaji.

Majukumu ya wawezeshaji katika mpango huu ni kama ifuatavyo:

a. Taasisi za kifedha

i. Kutayarisha mkopo (credit facility) au dhamana ya mkopo (credit guarantee) kwa chama husika au kwa msambazaji husika wa mbolea kulingana na masharti na taratibu zilizokubaliwa.

ii. Kutoa elimu na ushauri wa kitalaamu kwa wakulima wa kahawa juu ya masuala ya kifedha.

iii. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

b. Taasisi ya PASS (Private Agricultural Sector Support Trust)

Kutoa dhamana ya mikopo kwa vyama vya ushirika ambavyo havina uwezo wa kutoa dhamana ya kutosha kudhamini mikopo kwenye taasisi za fedha.

c. Makampuni ya usambazaji wa Mbolea

i. Kuingia makubaliano ya usambazaji wa mbolea iliyoanishwa kwa ajili ya kilimo cha kahawa katika eneo husika kwa wakulima wa kahawa kupitia vyama vya ushirika.

ii. Kutumia huduma za mkopo (credit facility) au dhamana ya mkopo (credit guarantee) zilizotayarishwa na taasisi za fedha ili kuhakikisha bei ya mbolea inakuwa nafuu.

iii. Kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya mbolea ikiwemo uanzishaji wa mashamba darasa, utunzaji na uhifadhi wa mbolea.

iv. Kushirikiana na taasisi ya utafiti wa kahawa TaCRI kufanya tafiti za mbolea zitakazotumika kwenye kilimo cha kahawa kulingana na maeneo.

v. Kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima wa kahawa kwa wakati kulingana na msimu wa kilimo na kama itakavyokuwa imeainishwa kwenye mkataba.

vi. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

d. Watoa huduma kwenye sekta ya kahawa Wanunuzi, Viwanda, Estates

i. Kuingia makubaliano na wakulima wa kahawa (Contract farming) itakayohusisha huduma ya upatikanaji wa mbolea.

ii. Makubaliano kati ya mtoa huduma na chama cha ushirika yatampa mtoa huduma nafasi ya kwanza ya kununua kahawa itakayozalishwa (first right of refusal).

iii. Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima.

iv. Kushirikiana na taasisi nyingine kufanya uhamasishaji wa matumizi bora ya mbolea.

v. Kutoa takwimu sahihi za fedha pamoja na pembejeo zilizogawanywa kwa wakulima kupitia vyama vyao vya ushirika.

3.7 Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC)

Ofisi ya Mrajis wa Ushirika kwa kupitia Warajis Wasaidizi wa Mikoa na Wilaya watakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kupitisha makubaliano ya mikopo ya mbolea kulingana na sheria inayoongoza vyama vya ushirika.
ii. Kuhakikisha vyama vya ushirika vinatoa takwimu sahihi za mahitaji ya mbolea.

3.8 Vyama Vikuu vya Ushirika na Vya Msingi (Unions) na AMCOS)

Majukumu ya vyama vya ushirika ni kama ifuatavyo:

i. Kukusanya na kuandaa mahitaji ya mbolea kwa wakulima kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo walio katika maeneo yao.
ii. Kufanya tathimini ya gharama na kiasi cha fedha kitakachohitajika kwa ajili ya ununuzi wa mbolea.
iii. Kuingia makubaliano na wawezeshaji/watoa huduma na wasambazaji wa mbolea kwa niaba ya wakulima.
iv. Kufanya tathmini ya watoa huduma/wawezeshaji juu ya gharama za huduma za mikopo ya mbolea ili kupata mtoa huduma mwenye gharama nafuu.
v. Kuhakikisha wakulima wa kahawa wanapata na kutumia kiasi cha mbolea kulingana na mahitaji waliyowasilisha.
vi. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

3.9 Mkulima

Majukumu ya wakulima katika utekelezaji wa mpango ni kama yafuatayo:

i. Kuandaa shamba kwa wakati kwa ajili uwekaji mbolea.
ii. Kuwasilisha mahitaji ya mbolea kwa watendaji wa vyama vya ushirika mapema.
iii. Kufuata na kupokea mbolea katika ofisi za vyama vya ushirika.
iv. Kutumia mbolea kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo kwa zao la kahawa na si vinginevyo.
v. Kuhudumia miti ya kahawa kwa kufuata kanuni bora za kilimo cha kahawa.
vi. Kuzingatia taratibu zote za uhifadhi wa mbolea kabla ya kuitumia shambani.
vii. Kufuata taratibu nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAMBO YA UJUMLA

4.1. Migogoro yoyote itakayojitokeza kati ya wakulima, taasisi za fedha, na wasambazaji wa mbolea itatatuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa Na. 23 ya mwaka 2001 pamoja na sheria nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4.2. Mwongozo huu utasomwa pamoja na Sheria ya Tasnia ya Kahawa Na. 23 ya mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2009 na Kanuni za Kahawa za mwaka 2013 na sheria inayosimamia masuala ya Mbolea Nchini

4.3. Mwongozo huu utatekelezwa na wadau wote waliotajwa kwenye mwongozo huu na endapo mtu yeyote atakiuka kutekeleza au kutenda kosa kwa mujibu wa mwongozo huu, atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria namba 23 ya Kahawa ya Mwaka 2001 na kanuni zake za mwaka 2013.

4.4. Ili kuleta uelewa wa pamoja bodi ya kahawa itaratibu kampeni za kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa wadau wa kahawa juu utekelezaji wa mwongozo huu.

4.5. **Usimamizi wa mpango, ufuatiliaji na tathmini.**

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango huu utakuwa kama ifuatavyo;

- Vyama vya ushirika vitawasilisha taarifa za utekelezaji wa mpango huu au upatikanaji wa mbolea kila mwaka mmoja (1).
- Bodi ya Kahawa katika hatua mbalimbali itafanya tathmini ya utekelezaji wa mpango kwa kuwashirikisha wadau wa kahawa ili kutambua mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu na kuzitafutia suluhisho.

Imetolewa na,

KAIMU MKURUGENZI MKUU,
BODI YA KAHAWA TANZANIA,
S. L. P 732,
MOSHI.